

USAWIRI CHANYA WA MWANAMKE KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARAB ZA BAKARI ABEID

Abdulrahaman Fayz Baheeri^{1*}, Mohamed Omary Maguo²

^{1,2} The Open University of Tanzania

*Corresponding: arhaim1991@gmail.com

الصورة الإيجابية للمرأة في أغاني "طرب" مختارة للفنان بكاري عبيد

عبد الرحمن فايز بحيري^{1*}، محمد عمري مغوو²
^{2,1} جامعة تنزانيا المفتوحة

Received: 27-03-2026; Accepted: 22-04-2026; Published: 13-05-2026

IKISIRI:

Makala haya yanahusu usawiri chanya wa mwanamke katika nyimbo za taarab za Bakari Abeid. Lengo kuu la makala lilikuwa ni kutaka kuchunguza namna mwanamke anavyosawiriwa katika hali chanya katika nyimbo za taarab za msanii maarufu za nyimbo za taarab anayefahamika kwa jina la Bakari Abeid. Makala yalikusanya data kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo na nadharia ya Ufeministi. Usawiri chanya wa mwanamke katika nyimbo za taarab za Bakari Abeid umejitokeza katika maeneo ya mwanamke kiumbe mwenye umbo zuri, mwanamke kiumbe mwenye msimamo, mwanamke kiumbe mwenye mapenzi ya kweli na mwanamke ni mtunza siri.

Keywords: Usawiri, Kiumbe, Chanya, Nyimbo, dhana.

المخلص

يتناول هذا المقال الصورة الإيجابية للمرأة في أغاني الطرب للفنان بكاري عبيد. هدف المقال الرئيسي هو دراسة كيفية تصوير المرأة بشكل إيجابي في أغاني الطرب للفنان الشهير بكاري عبيد. جمع المقال البيانات باستخدام منهج القراءة المتعمقة، وحللها باستخدام المنهج الوصفي والنظرية النسوية. برزت الصورة الإيجابية للمرأة في أغاني الطرب لبكاري عبيد في مجالات: المرأة كائن جميل، والمرأة كائن ذو مكانة قوية، والمرأة كائن يحب بصدق، والمرأة كحافظة أسرار

الكلمات المفتاحية: لوحة، مخلوق، ايجابي، اغنيه، مفهوم.

1.1 Utangulizi

Usawiri wa mwanamke katika kazi za kisanaa na zisizo za kisanaa imebebwa na dhana ya gainosentria (Gynosentrism) ambayo, kadiri ya Traore (2004), inalenga kupinga na kuhoja mfume dume katika uandishi ambapo mwanamke huwekwa kama dira ya yote yalio mema wakati mwanamke kusawiriwa kama mdhaifu, mkosaji na mkengeufu. Alijikita kuhamasisha uandishi wa kazi za fasishi ambapo mwanamke huwa kiini cha maudhui na pia kuchagiza uandishi wa kazi za Sanaa zinazofanywa na wanawake wenyewe na namna waandishi hawa wanavyosawiri wahuwika wa kike katika kazi zao toafuti na wale wa kiume.

Tafiti katika eneo hili zimeonesha kuwa wanawake husawiriwa kama jasiri; kwa mfano Aboye (h.t.) alichambua kazi mbili zilizotungwa na wanawake katika nchi za Afrika zilizo chini ya Jumuiya ya madola. Kazi hizo ni The Slave Girl ("Binti Mtumwa") na A Question of Power ("Swala la Madaraka"). Aliogundua kuwa wahuwika walikuwa wanawake jasiri waliobeba

majukumu ambayo kawida huhisiwa ni ya wanaume na lengo la waandishi likiwa ni kubadili fikra potofu kuhusu wanawake. Bazin (1989), kwa upande wake, alichunguza kazi za fasihi za watunzi wa Kiafrika Flora Nwapa, Buchi Emecheta, Bessie Head na Mafriana Ba. Alilenga utambuzi wa kifikra wa wahusika wa kike katika kazi za Sanaa za hao waandishi. Aligundua kwamba kwa ujumla kazi zote zimedhihirisha kuwepo kwa nyakati za dhiki na mateso kwa wahusika wanawake ila hao wahusika walibaki imara, wenye nguvu na hodari dhidi ya madhila yaliyowakuta.

Pia Straton (1994) alitathmini kazi za sanaa za Grace Ogot, Mariama Ba, Flora Nwapa, na Buchi Emecheta, ambao ni waandishi wanawake wa Africa na kung'amua kwamba waandishi wenyewe wanakuwa katika hali ya njia panda ya undimila kuwili wa jamii kuwa kioo kinachangaza yaliyomo kwenye jamii (hata yenye uonevu na ukakasi wa kimaadili), kwa upande mmoja, na kuwa mwanga unaonesha njia mbadala na sahihi (hata kama inakinzana na wimbi la imani na tamaduni za jamii. Makala haya yanaangazia usawiri wa mwanamke katika nyimbo za taarab za Bakari Abeid ambaye ni mwimbaji wa nyimbo za taarab asilia kutoka Zanzibar.

2.1 Maana ya Taarab Asilia

Taarab asilia si muziki wa kucheza bali wa kutazama, kusikiliza, kutafakari na kutunza. Taarab ni muziki ambao hutungwa kwa kutumia lugha ya mafumbo ambayo hauzuii familia, (mfano baba, mama na mtoto) kuweza kufanya washindwe kutazamana au kusikiliza. Vilevile, unatumia ala kama vile fidla, dumbaki, ganuni, kinanda na dabalibesi ambazo hutoa muziki mororo unaofanya msikilizaji au mtazamaji atikise kichwa au kucheza vidole polepole (Makila, 2011). Kwa sasa taarab asilia inapigwa na vikundi vya Culture Musical Club na Ilias and Twinkling Stars huko Stone Town Zanzibar, na kikundi cha Sanaa ya Taarab katika kijiji cha utalii kilichopo Nungwi Zanzibar kwa ajili ya watalii wanaotembelea kisiwa hicho wakati wa kiangazi (Traore, 2004), Katika tafiti tangulizi, **Khadija Abdallah Kisarazo, Mohamed Omary Maguo na Felistas Richard Mahong** (2025) walichunguza ubainishaji wa kejeli katika nyimbo za taarab za **Khadija Kopa**. Utafiti wao ulibaini kuwa nyimbo hizo zimejaa kejeli mbalimbali zinazotumiwa kufikisha ujumbe wa kijamii kwa hadhira. Hata hivyo, utafiti huo ulijikita katika kejeli, hivyo kuacha pengo la kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke katika nyimbo za taarab.

3.1 Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yameongozwa na nadharia ya Ufeministi ambayo kwa mujibu wa Birk (1986) anaeleza kuwa ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbalimbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Nadharia ya Kifeministi ilianza kuzungumzwa katika karne ya 19 na kutia fora miaka ya 1960 na 1970. Katika wakati huu wamagharibi walianza kuzungumzia matatizo yao katika machapisho na kufichua matatizo yanayowapata kama tabaka la kiuchumi na pia kama wanawake (Wafula na Njogu 2007). Wamitila (2002) anaeleza kuwa nadharia ya Kifeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 huko Ulaya, hususan katika nchi za Uingereza na Marekani. Katika kipindi hicho wanawake hawakuthaminiwa katika jamii zao na walikuwa ni watu waliokuwa katika daraja la chini. Vilevile, wanawake hawakuhusishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile kupiga kura au kuchaguliwa katika uongozi. Sehemu iliyoonekana hasa kuwafaa wanawake ni katika shughuli za jikoni. Unyanyasaji huu wa wanawake ndio uliopelekea kuibuka kwa nadharia hii ya kifeministi.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa baadhi ya kazi za mwanzo kuyafafanua masuala ya wanawake kinadharia ni A Vindication of the right of a woman (1792) ya Mary Wollstonecraft. Pia kazi nyingine ni The Second Sex (1952) ya Simone de Beauvoir ambaye alikosoa na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke, kama vile dini, ndoa na utamaduni. Kwa mujibu wa Wamitila, Simone de Beauvoir anaeleza kuwa utamaduni

anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kukubali hali hiyo, mwanamke anaishia kuwa chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo. Mfano, ndoa ni asasi mojawapo ya kiutamaduni inayoendeleza ukandamizaji wa wanawake ambayo inamjenga kwenye imani na uwezo mkubwa alionao mwanaume na kuishia kumuangalia mwanamke kama chombo tu. Nadharia hii ni mufaka katika kufanikisha uchambuzi wa data za makala haya ambazo zinahusu usawiri wa mwanamke katika nyimbo za taarab za Bakari Abeid kwa kurejelea baadhi ya nyimbo zake chache. Pamoja na mambo mengine, nadharia hii inalenga kumkomboa mwanamke kutokana na unyanyasaji anaofanyiwa katika jamii kupitia mfumo dume uliotawala katika jamii nyingi za Kiafrika na dunia kwa jumla.

4.1 Methodolojia ya Makala

Makala haya yanakusudia kupata data kutoka katika nyimbo za taarab za Bakari Abeid zenye kukidhi malengo ya makala haya ambayo ni kuchunguza usawiri wa mwanamke katika nyimbo za taarab asilia za Bakari Abeid. Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini ambapo mtafiti alipakuwa nyimbo za Bakari Abeid kutoka katika mitandao na kisha kuzisoma kwa makini nyimbo hizo kwa lengo la kupata data. Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kwa mtafiti kusoma matini yenye maandishi kwa umakini wa hali ya juu kwa lengo la kupata data (Kothari, 2004; Kombo na Tromp, 2006). Kupitia mbinu hii mtafiti alikusanya data kwa kuzingatia hatua tano ambapo hatua ya kwanza ilikuwa ni kusoma mashairi ya nyimbo za Bakari Abeid kwa mara ya kwanza bila kuchukuwa nukuu au dondoo lolote, hatua ya pili ilikuwa ni kusoma na kuanza kudondoa, hatua ya tatu ikawa ni kuaandaa mada na vichwa kwa ajili ya kuweka data za madondoo, hatua ya nne ikawa ni kupanga data kwa kuweka zinazofanana pamoja na kutenganisha zinazotofautiana na hatua ya tano ikawa ni kupangilia data katika mpango rahisi wa kuzichambua. Data za utafiti zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo ambapo mtafiti aliandaa vichwa na kuvipa madondoo kwa ajili ya uchambuzi kwa mujibu wa mada ya makala, kisha alitoa ufafanuzi wa kila dondoo kwa namna inayojibu hoja ya makala, baadaye akahusisha nadharia katika uchambuzi na mwisho atajenga hoja na kuihitisha kisha kwenda kwenye hoja nyingine. Usomaji makini pamoja na mbinu ya kimaelezo ni methodolojia muafaka ambazo ziliwezesha kukamilika kwa makala haya.

5.1 Usawiri wa Mwanamke

Mwanamke katika kazi za fasihi amekuwa akisawiriwa kwa namna mbalimbali lakini hali hali ikijitokeza kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na hali chanya.

5.1.1 Mwanamke na Umbo zuri

Msanii Bakari Abeid anamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye umbo zuri la kuvutia watu na hasa wanamume. Haya yanapatikana katika wimbo wake wa “Kiumbe Nimpendaye,” kama unavyodondolewa baadhi ya beti hapa chini:

Kiumbe nimpendae, mzuri aloumbika
Tofauti mimi naye, ni rangi zetu na myaka
Hakuna amjuaye bure mtahangaika

Katika dondoo hili mwanamke ambaye anapendwa ni yule ambaye ana umbo zuri pamoja na viuongo vyake vingine vya mwili vikiwa ni vyenye kuvutia. Mwanamke pia anasawiriwa kama kiumbe msafi na mrembo kitu ambacho kila mwanamke anapenda kusifiwa nacho. Wanaufeministi hawana tatizo na mwanamke kusifiwa kuwa na umbo zuri bali tatizo walilionalo ni kuona mwanamke anatazamwa kama chombo cha starehe kutokana na maumbile yake. Kumtumia mwanamke kama chombo cha starehe ni unyanyasaji wa kijinsia na kumdhaliisha mwanamke.

5.1.2 Mwanamke ni kiumbe mwenye msimamo

Msanii Bakari Abeid anamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye msimamo katika jamii ambaye anaweza kukabiliana na hali mbalimbali katika mazingira yake yanayomzunguka. Tuone dondoo kutoka wimbo wa “Pendo silitoi ovyo”

Pendo silitoi ovyo, nimpaye humpima
Alonikalia sivyo, sichelewi kumnyima
Alonikalia ndivyo, nampa sirudi nyuma

Wengi walifanya pupa, njama zao zikakwama
Na viapo waliapa, walipate kwa lazima
Wameliacha hapahapa, kwangu linawatazama

Dondoo hili linamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye msimamo katika mapenzi ambapo hatoi penzi hovyoy hovyoy bali kwa mpenzi wake tu na siyo mtu mwingine. Katika dondoo inaonekana wapo wanamume wamekuwa wakimhadaa mwanamke ili akubali kufanya nao mapenzi lakini mwanamke ameonesha msimamo wake thabiti wa kutohadaika. Huu ni mfano mzuri sana kwani baadhi ya wanajamii hudhani kwamba mwanamke ni kiumbe wa kudanganywa tu na kudanganyika. Kwa mujibu wa nadharia ya Ufeministi mara zote mwanamke ni kimube mwenye msimamo na kutokana na msimamo wake thabiti amekuwa ni chanzo cha ustawi wa mwanamume pamoja na familia ila tu wapo baadhi yao wachache wenye hulka na tabia zao mbaya kama ilivyo kwa wanamume pia.

5.1.3 Mwanamke ni kiumbe mwenye mapenzi ya Kweli

Msanii Bakari Abeid kupitia nyimbo zake za taarab anamsawiri mwanamke kama mtu mwenye kusema ukweli daima katika maisha yake. Tuone mfano kutoka katika wimbo wa “Sikitiko la Daima,” kama ifuatavyo:

Natoa yangu kauli, unisikie azizi
Mwenginewe sibatili, jambo hilo siliwezi
Moyo wangu ni jabali, hauvuji upuuzi

Kiitikio:
Moyo wangu ni jabali, hauvuji upuuzi
Yaniadhibu mapenzi, tabibu wangu ni wewe

Ahadi tulopeana, zimeshatoa mizizi
Mengi tuloambizana, ya furaha na simanzi
Hapana alotuona, ushahidi mbalamwezi

Kiitikio:
Hapana alotuona, ushahidi mbalamwezi
Yaniadhibu mapenzi, tabibu wangu ni wewe

Dondoo hili linamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye mapenzi ya kweli kwa mwanamume kiasi kwamba mme anaeleza waziwazi kwamba hawezi kumuacha mwamake huyo kutokana na mapenzi yake ya kweli aliyonayo. Mwanamume anaeleza pia, kwamba hata anapokuwa katika kazi ngumu zenye maumivu hachoki kwa sababu anajua akirui nyumbani atakutana na mke mwenye mapenzi ya kweli na itakuwa ni faraja na uchovu wote utaondoka. Wanaufeministi wanaeleza kwamba, mwanamume anapokuwa na amani ya moyo anaweza kufanya kazi kwa kujituma sana ili kuweza kutimiza malengo yake na inapokuwa ni kinyume

basi ni rahisi sana kwa mwanamume kushindwa kufanya kazi kutokana na msongo wa mawazo. Mapenzi ya kweli ya mwanamke kwa mwanamume ni silaha ya kumtuliza mwanamume na kumpa nguvu ya kujituma zaidi katika kufanya kazi. Katika jamii wapo baadhi ya wanamume ambao wamepoteza mwelekeo kutokana na kukosa wanawake wenye mapenzi ya kweli na kuwasababishia hata kuharibu kazi zao.

5.1.4 Mwanamke mtunza siri

Kutunza siri ni jambo kubwa sana kwa binadamu kwani wengi wameshindwa kutunza siri na kuwa ni watu wa kueleza hata mambo ya ndani ya nyumbani kwao kwa watu wengine wasiohusika. Tuone mfano katika wimbo wa “Yu wapi wangu Muhibu,” kupitia dondoo lifuatalo:

Liloniathiri, siwezi kutaja
Atowaye siri, huwa hana hoja
Tandoa nadhiri, utakapokuja

Katika dondoo hili kunaoneshwa kwamba mwanamke siyo kiumbe wa kutoa siri bali mtunza siri kwa sababu mwenye kutoa siri huwa hana hoja bali ana viroja. Kutunza siri kunajenga heshima ya mwanamke na yule ambaye hatunzi siri hukosa heshima katika jamii kwani watu humuona kama mtu asiyeaminika. Wana Ufeministi wanaeleza kwamba, miongoni mwa viumbe wenye uwezo mkubwa wa kutunza siri ni wanawake nah ii inathibitishwa na mambo mengi ambayo wanafanyiwa katika jamii lakini wanavuiliana na kutunza siri. Wanatoa mfano wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kuwa ni moja kati ya vitu ambavyo wanawake wengi wanafanyiwa hata na ndugu wa karibu lakini wanaweka siri na kutokueleza kwa watu. Hivyo kutunza siri ni sifa ya mwanamke ingawa wapo wachache ambao hawatunzi siri bali kazi yao ni kuona ufahari kueleza mambo yao ya ndani kwa watu wengine wasiohusika.

6.1 Hitimisho

Makala haya yameonesha kwamba mwanamke amesawiriwa katika hali chanya kupitia nyimbo za taarab za msanii Bakari Abeid ikiwa ni ithibati kwamba mwanamke ni kiumbe muhimu katika maisha na ustawi wa familia na jamii kwa jumla. Miongoni mwa sifa alizosawiriwa nazo mwanamke ni kuwa na umbo zuri, mwanamke ni kiumbe mwenye msimamo, mwanamke ni kiumbe mwenye mapenzi ya kweli na mwanamke ni mtunza siri. Kwa hakika usawiri huu wa mwanamke katika hali chanya ni kitu ambacho Wanaufeministi wanakipigania sana kama sehemu ya kumkomboa mwanamke. Ukombozi wa mwanamke ni harakati ya muda mrefu na itafanikiwa ikiwa wanajamii wote wakiwemo wasanii watamsawiri mwanamke katika hali chanya na kuiona hali hasi kama sehemu tu ya ubinadamu na siyo kwamba ndiyo silica na hulka ya mwanamke. Kutoakana na ukweli huu, hivi sasa wanawake wanang'ara sana katika jamii kwani wameshika nafasi mbalimbali za uongozi katika jamii na wanaongoza vizuri sawasawa na wanamume na katika baadhi ya mazingira wakifanya vizuri kuliko wanamume.

VIAMBATANISHO: NYIMBO TEULE ZA BAKARI ABEID

1: SIKITIKO LA DAIMA

Sikitiko sikitiko, la daima na majonzi
Sura na wajihi wako, hunijia kwenye njozi
Nisaidie mwenzako, wewe ndiye mpumbazi

Kiitiko

Nisaidie mwenzako, wewe ndiye mpumbazi

Yaniadhibu mapenzi, tabibu wangu ni wewe
Mapenzi haya ya kweli, mimi bado mwanafunzi
Walahi yananidhili, umenishia ujuzi
Kumbe ni sumu katili, na kuitema siwezi

Kiitikio

Kumbe ni sumu katili, na kuitema siwezi
Yaniadhibu mapenzi, tabibu wangu ni wewe

Natoa yangu kauli, unisikie azizi
Mwenginewe sibatili, jambo hilo siliwezi
Moyo wangu ni jabali, hauvuji upuuzi

Kiitikio

Moyo wangu ni jabali, hauvuji upuuzi
Yaniadhibu mapenzi, tabibu wangu ni wewe

Ahadi tulopeana, zimeshatoa mizizi
Mengi tuloambizana, ya furaha na simanzi
Hapana alotuona, ushahidi mbalamwezi

Kiitikio

Hapana alotuona, ushahidi mbaramwezi
Yaniadhibu mapenzi, tabibu wangu ni wewe

2: PENDO SILITOI OVYO

Pendo silitoi ovyo, nimpaye humpima
Alonikalia sivyo, sichelewi kumnyima
Alonikalia ndivyo, nampa sirudi nyuma

Kiitikio

Ooooh! Ooooh! ha! ha! ha! ha!

Humpa mwenye mahaba, ya kweli na taadhima
Raha zake kwangu tiba, narahika akisema
Pendo langu ni la hiba, si la fujo na lawama

Kiitikio

Ooooh! Ooooh! ha! ha! ha! ha!

Humpa mwenye murua, mtu mwenye sifa njema
Kwa uradhi hulitoa, humpa mwenye heshima
Sina choyo kulitoa, kumpa mwenye hekima
Simpia alogombaniwa, na watu chungu mzima

Kiitikio

Ooooh! Ooooh! ha! ha! ha! ha!

Wengi walifanya pupa, njama zao zikakwama

Na viapo waliapa, walipate kwa lazima
Wameliacha hapahapa, kwangu linawatazama

Kiitikio

Ooooh! Ooooh! ha! ha! ha! ha!

3: YU WAPI WANGU MUHIBU

Yu wapi muhibu, wangu simuoni
Ninamtafuta, hatoki moyoni
Haya ni maradhi, katu hayaponi

Kiitikio

Ho! ho! ho! ho! ha! ha! ha! ha!

Ni lipi Habibi, nililokuudhi
Lipi ninenalo, nisilokuridhi
Kukunyenyekoa, kwangu ni faradhi

Kiitikio

Ho! ho! ho! ho! ha! ha! ha! ha!

Silaumu mtu, wala wangu moyo
Hakuna kiumbe, asofikwa hayo
Wapi umekwenda, niifate nyayo

Kiitikio

Ho! ho! ho! ho! ha! ha! ha! ha!

Liloniathiri, siwezi kutaja
Atowaye siri, huwa hana hoja
Tandoa nadhiri, utakapokuja

Kiitikio

Ho! ho! ho! ho! ha! ha! ha! ha!

4: KIUMBE NIMPENDAYE

Kama kupenda ni dhara, mwezenu nimedhurika
Nnapenda kwa ishara, naogopa kutamka
Naichelea idhara, nakuja kufedheheka

Kiitikio

Mwenzenu nimedhurika wala sina manusura
Naogopa kutamka, naichelea idhara

Kiumbe nimpendaye, mzuri aloumbika
Tofauti mimi naye, ni rangi zetu na myaka
Hakuna amjuaye, bure mtahangaika

Kiitikio

Mwenzenu nimedhurika wala sina manusura
Naogopa kutamka, naichelea idhara

Nyusi zake za kifungo, na pua imenyooka
Miguu yake na shingo, kwa yeyote huvutika
Mcheshi hana maringo, akiudhiwa hucheka

Kiitikio

Mwenzenu nimedhurika wala sina manusura
Naogopa kutamka, naichelea idhara

Si mfupi si mrefu, kimo chake muafaka
Maridadi si mchafu, mrembo wa kusifika
Kwa heshima hana hofu, popote atizamika

Kiitikio

Mwenzenu nimedhurika wala sina manusura
Naogopa kutamka, naichelea idhara.

MAREJELEO

- Bazin, N. T. (1989) "Feminism in the Literature of African Women." *The Black Scholar*, 20(3-4), 8-17.
- Birk, L. (1986) *Woman Feminism and Biology: The Feminist Challenge*, Brogton: Wheatsheal.
- Khadija Abdallah Kisarazo, K. A., Mohamed Omary Maguo, M. O., & Felistas Richard Mahong, F. R. (2025). Ubainishaji wa kejeli zilizomo kwenye nyimbo za taarab za Khadija Kopa. *East African Journal of Swahili Studies*, 8(1), 1–16.
- Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A (2006) *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Pauline's Publications.
- Kothari, C. R. (2004) *Research Methodology, Methods and Techniques*. Second Edition, Delhi: New Age International (P) Ltd.
- Massoud, S. R. (2022) "Kuchunguza taswira katika nyimbo za taarab za Kimahaba za Khadija Kopa." *Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*.
- Makilla S. (2011) <http://fitimbaeafrika.blogspot.com/2011/06/taarabu-asilia-ni-urithmusiopotea.html> imesomwa 6/10/2012
- Stratton, F. (1994) *Contemporary African literature and the politics of gender*. London: Routledge.
- Traore, F. A. (2004) *Continuity and Change in Zanzibar Taarab Performance and Poetry*, *Swahili Forum* 11,75-84.
- Wafula, R. M na Njogu, K (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wendo, F. & Titus, K. (2025) "Maudhui ya Ukungwi katika nyimbo teule za Taarab," katika *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 8(2), kur. 119-132.

Disclaimer/Publisher's Note: The statements, opinions, and data contained in all publications are solely those of the individual author(s) and contributor(s) and not of **AJHAS** and/or the editor(s). **AJHAS** and/or the editor(s) disclaim responsibility for any injury to people or property resulting from any ideas, methods, instructions, or products referred to in the content.